88142316

International Baccalaureate®
Baccalauréat International
Bachillerato Internacional

**SWAHILI B – HIGHER LEVEL – PAPER 1**
**SWAHILI B – NIVEAU SUPÉRIEUR – ÉPREUVE 1**
**SWAHILI B – NIVEL SUPERIOR – PRUEBA 1**

Wednesday 12 November 2014 (morning)
Mercredi 12 novembre 2014 (matin)
Miércoles 12 de noviembre de 2014 (mañana)

1 h 30 m

---

TEXT BOOKLET – INSTRUCTIONS TO CANDIDATES

- Do not open this booklet until instructed to do so.
- This booklet contains all of the texts required for paper 1.
- Answer the questions in the question and answer booklet provided.

LIVRET DE TEXTES – INSTRUCTIONS DESTINÉES AUX CANDIDATS

- N'ouvrez pas ce livret avant d'y être autorisé(e).
- Ce livret contient tous les textes nécessaires à l'épreuve 1.
- Répondez à toutes les questions dans le livret de questions et réponses fourni.

CUADERNO DE TEXTOS – INSTRUCCIONES PARA LOS ALUMNOS

- No abra este cuaderno hasta que se lo autoricen.
- Este cuaderno contiene todos los textos para la prueba 1.
- Conteste todas las preguntas en el cuaderno de preguntas y respuestas.


© International Baccalaureate Organization 2014

https://xtremepape.rs/

**KIFUNGU A**

# AJALI YA BASI YAUA WATU 16 TANGA

Watu 16 wamekufa na wengine zaidi ya 93 kujeruhiwa vibaya baada ya basi la Kampuni ya Burudani walilokuwa wakisafiria kupinduka katika kona ya Kwaluguru kata ya Kwedizinga wilayani Handeni Mkoani Tanga. Ajali hiyo ilitokea jana saa moja na nusu asubuhi ambapo basi hilo linalofanya safari zake kati ya Korogwe na Dar es Salaam kila siku, linadaiwa lilikuwa katika mwendo wa kasi uliosababisha dereva wake kushindwa kulimudu na kuacha njia. Akithibitisha kutokea kwa ajali hiyo, Kamanda wa Poilisi Mkoa wa Tanga, Constantine Massawe, alisema gari hilo aina ya Nissan Diesel, lilikuwa likitokea Korogwe kuelekea Dar es Salaam nchini Tanzania lilikuwa likiendeshwa na dereva Luta Mpenda ambaye naye alikufa papo hapo katika eneo la ajali.

**Matibabu ya waliojeruhiwa**

Kamanda Massawe alisema, majeruhi wote waliopata ajali walikimbizwa katika Hospitali ya Magunga wilayani Korogwe kwa ajili ya matibabu zaidi. Alisema kutokana na ukubwa wa tatizo hilo, wameomba msaada wa madaktari kutoka hospitali ya mkoa ya Bombo ili kuweza kuokoa maisha ya watu hao. "Ni ajali mbaya sana na hivi sasa tunavyozungumza, nipo katika eneo la ajali tukiangalia uwezekano wa kuomba msaada wa madaktari kutoka hospitali za mkoa ili kuokoa maisha ya majeruhi walioumia kwa kiasi kikubwa", alisema Kamanda Massawe.

Akizungumza hapo hospitalini, Kaimu Daktari Mkuu wa Hospitali ya Wilaya Korongwe, Dkt. Simon Mngulwi, alithibitisha kupokea majeruhi 93 wa ajali hiyo huku wengine 16 wakipoteza maisha yao. "Tumepokea majeruhi 93 kati ya hao 50 ni wanawake na 43 ni wanaume na kati yao 19 wako katika hali mbaya sana pamoja na hali hii bado tunakabiliwa na uhaba wa damu na tumeomba msaada kutoka hospitali ya mkoa ya Bombo "Abiria kumi wamehamishwa hadi hospitali mbili za rufaa", alisema Dkt. Mgulwi. Hata hivyo alisema maiti zilizopelekwa katika hospitali hiyo ni 12 ambazo kati yazo ni: wanaume sita, watoto watatu na wanawake wawili huku maiti moja ikiwa bado haijatambuliwa kutokana ajali hiyo mbaya.

**Shahidi akumbuka**

Akisimulia namna ajali hiyo ilivyotokea, mmoja wa majeruhi waliolazwa katika hospitali hiyo, Pamela Msondo alisema gari lilikuwa limejaza watu kupita uwezo wake wa kawaida huku abiria wengine wakilazimika kusimama. "Tulipofika kwenye kona ya Kwaluguru ndipo tulipokutana na gari ambalo lilikuwa linapita gari lingine kwa hivyo ili kuepuka kugongana uso kwa uso, ndipo dereva alichipukia kando ya barabara na kuangukia upande na kupinduka. Tuna bahati kuwa hai", alisema Msondo.

Imetoholewa kutoka John Ngunge, *Rai* (2013)



https://xtremepape.rs/

**KIFUNGU B**

## KAMPUNI YALETA MAPINDUZI YA ELIMU



Wakati dunia ikiwa kwenye shughuli mbalimbali za kitaaluma za elimu, hatimaye Kampuni mashuhuri imeanzisha programu mpya ambayo itawawezesha wanafunzi kufanya mazoezi yote wanayopewa shuleni kupitia mfumo wa teknolojia mpya. Programu hii itawawezesha wanafunzi kupeana kazi za shule, mazoezi ya nyumbani na maswali yote muhimu ya kitaaluma.

Mpango huo ulitangazwa mapema wiki hii na kampuni hiyo wakati ikitambulisha masomo ya teknolojia ambayo inakadiriwa kutumiwa na zaidi ya wanafunzi milioni 110 duniani. Programu hiyo itawapa wanafunzi fursa ya kuitumia kupitia huduma zilizopo kama vile kugawana stakabadhi, kuzihifadhi na barua pepe bila malipo.

Mpango wa kutumia programu hiyo ulianza rasmi Desemba mosi mwaka huu, huku vyuo mbalimbali duniani vikipewa leseni bila malipo yoyote. Huduma hizo zote zitawapa wanafunzi nafasi ya kupata maarifa mbalimbali kupitia mtandaoni wakiwa nyumbani pamoja na huduma nyingine ambazo zipo kwenye programu hiyo yenye vitu vingine vitakavyomwezesha mwanafunzi kuwasiliana na wanafunzi wengine katika vyuo mbalimbali duniani. Wanafunzi watakaotumia huduma hii kila siku wataweza kufanya kazi zao nyingi za shule na zile muhimu kwa kutumia programu hiyo spesheli.

"Hii itawasaidia wanafunzi kujumuika pamoja katika kazi zao za vyuoni na kuongeza ufanisi wao kitaaluma", asema meneja wa kampuni hiyo. Kwa mujibu wa taarifa iliyotolewa, wamefanikiwa kutembelea vyuo 30 vya kibinafsi na vya umma pamoja na wizara mbalimbali za elimu ili kutoa mafunzo ya juu ya kutumia programu hiyo.

Anasema mpango huo upo chini ya kampuni ya Data ambayo itakuwa ikikusanya taarifa za maendeleo ya wanafunzi mbalimbali watakaoitumia ili waweze kupata ajira na kuboresha maisha yao.

Kampuni hiyo inasema inakusudia kufuatilia uwezo wa wanafunzi katika kutumia huduma hiyo. Wale watakaoonekana kuwa na kiwango cha juu watachukuliwa na kupelekwa kwa makampuni mbalimbali na kulipwa mishahara minono. Kampuni hiyo imepanga kutengeneza ajira kwa asilimia 28 ifikapo mwaka wa 2020 ambapo miongoni mwa wanafunzi milioni 115 watakaoajiriwa kwa namna zilizowekwa. "Walimu wanapaswa kubuni njia mpya za kufundisha wanafunzi wao ili kuboresha sekta ya elimu."

"Elimu ya mawasiliano ya teknolojia ni muhimu kwani inarahisisha utendaji wa kazi na kuongeza uwezo wa wanafunzi wote watakaofaulu kuingia kwenye soko la ajira sasa na baadaye", asema, Meneja wa kampuni hiyo.

Imetoholewa kutoka Markus Mpangala, *Rai* (13 Desemba 2013)



https://xtremepape.rs/

**KIFUNGU C**

## SERIKALI IMEAMUA KUSHINDWA VITA DHIDI YA DAWA ZA KULEVYA?




Wiki mbili zilizopita, niliandika katika safu hii kuhoji ni kwa namna gani kilo 150 za dawa za kulevya, zilipitishwa katika Uwanja wa Kimataifa wa Julius Nyerere jijini Dar es Salaam bila kubainika. Dawa hizo, zilizokuwa zinasafirishwa na wasanii wawili, zilikamatwa katika uwanja wa ndege huko Afrika Kusini. Kwa namna yoyote ile, kitendo hicho kinaonyesha udhaifu usiopimika na kutokuwepo kwa utayari katika sehemu kubwa ya vyombo husika kupiga vita dawa za kulevya.

Siyo rahisi kuelewa ni kwa nini na ni kwa namna gani mtu anaweza kupitisha kiwango kidogo tu cha dawa za kulevya katika eneo ambalo lina kila aina ya ulinzi na ukaguzi kama kiwanja cha ndege cha kimataifa. Inashangaza zaidi pale kiwango hicho cha dawa kinachopitishwa bila kubainika kikiwa ni kiwango kinachofikia kilo 150! Tukio hilo lilionyesha kuwa hatuko salama kama nchi. Kama eneo kuu la mpaka la uwanja wa kimataifa, linaweza kutumika kupitisha kiwango kikubwa kama hicho cha dawa za kulevya, ni nini kitawazuia watu wenye nia mbovu kupitisha vitu vingine ambavyo vinaweza kuidhuru nchi na watu wake?

Kama wafanyakazi wa uwanjani humo wameacha kilo 150 za dawa za kulevya zikapita vivi hivi, ni nini kitawawezesha kuzuia wasiachie vitu vingine kupita? Lakini jambo hilo ni kielelezo tu cha jinsi tulivyoshindwa kuilinda nchi yetu dhidi ya wafanyabiashara wa dawa za kulevya. Uthibitisho zaidi ni matukio mengine kadhaa yaliyotokea baada ya tukio hilo.

Mara baada ya tukio hilo, ikaibuka barua inayoelezwa kuwa imeandikwa na mmoja wa vijana waliokamatwa huko Hong Kong wakiwa na dawa za kulevya na kufungwa. Kati ya mambo mengi aliyoeleza kwenye barua hiyo, kijana huyo ambaye hajitaji jina lake anatoa orodha ya wafanyabiashara wanaojihusisha na biashara hiyo haramu.

Mkuu wa kitengo cha kupambana na dawa za kulevya, Kamishna Msaidizi wa Polisi, Godfrey Nzowa, anabainisha kuwa ni kweli baadhi ya majina yaliyomo kwenye orodha hiyo wao wanayo. Lakini maelezo ya Nzowa yanaonyesha kuwa Jeshi la polisi na kitengo chake, kimeshindwa kupambana na wafanyabiashara hao licha ya kufahamika.



https://xtremepape.rs/

Mathalani, anabainisha kuwa kitengo chake kilishawahi kuwafikisha mahakamani baadhi ya wafanyabiashara hao. Lakini badala ya kuwashitaki kwa makosa yanayohusiana na biashara ya dawa za kulevya, waliiomba mahakama iwaweke watu hao chini ya uangalizi wake. Hii inamaanisha kuwa wakati wanawapeleka mahakamani, Jeshi la Polisi halikuwa na ushahidi usio na shaka kuhusiana na uhusika wa watu hao kwenye biashara hiyo. Hivyo, ruhusa ya kutaka wawe chini ya uangalizi wao, inamaanisha kuwa wanataka kuwachunguza ili wapate ushahidi dhidi yao.

Hili ni jambo la ajabu. Yaani umwambie mwizi kuwa sasa yupo chini ya uchunguzi ukitarajia kweli katika kipindi hicho atakwenda kuiba ili upate ushahidi wa wizi dhidi yake! Na hicho ndicho kilichotokea. Hakuna ushahidi uliopatikana dhidi ya wale waliowekwa chini ya uchunguzi hadi leo hii. Na baadhi ya watu hao tayari wameshatoroka nchini.

Imetoholewa kutoka Esther Mbussi, *Mtanzania* (2013)





https://xtremepape.rs/

**KIFUNGU D**

## ATHARI ZA MAISHA YA KISASA

*Juma alikuwa: mrefu, mweusi, mtanashati na mkwasi. Alikuwa na ladha ya magari, saa na zaidi ya yote wanawake. Monika alikuwa msichana mrembo aliyekuwa amefuzu kutoka Chuo Kikuu. Halikuwa jambo la kushangaza kwa mwanaume kama Juma kumtambua. Rashid alikuwa mwangalifu, anayelinda mno Monika msichana mrembo aliyeishi naye baada ya msichana huyo kutoroka nyumbani kwao baada ya kukosana na wazazi wake.*

Siku ile Juma aliazimia kumwalika Monika (mpenziye) katika densi kubwa itakayopigwa katika hoteli moja, ambayo kwa siku nyingi ilikuwa ikitangazwa. Alielewa kuwa muziki utakuwa wa kufurahisha na alivyokuwa akijua kuwa hataweza kulala kwa fikira zake nyingi, aliona bora kukesha katika dansi hiyo. Pia aliona kuwa Monika atafurahi. Aliinua simu na kumpigia Monika kazini kwake ili kumwarifu hayo mapema.

Tokea siku ile Monika alipokutana na Juma, alikuwa kila siku yumo katika safari na matembezi. Kwa muda wa wiki mbili Monika alitembezwa kwa gari na Juma. Alikuwa kijana aliyevalia vizuri wakati wote. Wakati mwingine Monika alikuwa na shaka kuwa anavalia vizuri sana, hata ijapokuwa wakati hauhitaji. Saa za jioni pia, wakati joto lilikuwa jingi, Juma siku zote alikuwa amevalia suti kamili, kama ambaye halihisi joto lile hata kidogo.

Rashid wakati wote huo alikuwa akimtahadharisha Monika dhidi ya tabia ya kutokatoka pekee, hasa usiku, lakini Monika alihesabu hiyo ni gere ya Rashid. Kwa hivyo alizidi kufurahi kwa kuweza kumkera kila siku.

Siku ile Monika aliagana na Juma saa za jioni wakati anapotoka kazini. Waliagana kwenda kula chakula katika hoteli mojawapo na baadaye waende sinema. Monika alikubali hayo kwa furaha na asubuhi alipotoka alivalia kwa madhumuni hayo. Alimwachia Rashid kikaratasi juu ya meza ya kulia. "Nitakawia kurudi. Pengine nitarejea usiku, Monika".

Rashid alipokuwa akitoka, huku akimeza funda la chai ya moto kwa haraka na ambayo ilikaribia kumbambua, alikiona kile kikaratasi. Alikichukua na kukisoma, tena akikiviringa viringa mkononi na kukitupa katika debe la taka alipotoka nje, huku akisema "Sijapata kuona asiyesikia kama huyu, lakini hiari yake". Waswahili wamesema, "Mtoto akicheza na moto atachomeka". Alianza kuhangaika kutafuta ufunguo wake wa gari mfukoni na alipoupata alifungua mlango, akavurumisha mkoba wake ndani, akaingia na kutia gari moto kwani alikuwa amechelewa.

Alipofika kazini alihisi kuna jambo fulani lililotokea na lililomhusu yeye, lakini hakulijua ni lipi. Alipojiuliza alijuaje, alijiambia labda kwa namna wale wenzake walivyokuwa wakimtazama, au wanavyozungumza na yeye kwa sauti kubwa isiyohitajika, kama watu wanaojaribu kuficha jambo fulani lililomo vichwani mwao na wanaogopa wakinyamaza ua kutulia yeye ataweza kuiona siri hiyo. Hakujua hasa ni jambo gani na kiburi chake hakikumruhusu kuuliza mtu yeyote, ila alihisi kuwa kulikuwa na mabishano makubwa kumhusu yeye.

Zeinab Burhani, *Mwisho Wa Kosa* (2007)



https://xtremepape.rs/

**KIFUNGU E**

## Wanyama wetu wa pori wanaopungua




Silaha za atomatiki zinadunga kupitia kwa mbuga ya kitaifa ya wanyama ambayo ni Tsavo Mashariki nchini Kenya. Waathiriwa wanaolengwa ni ndovu wachache. Yule binadamu mlinzi yuko mbali sana kuwaona au kuwasikia wakianguka na kugaagaa kwa maumivu mmoja baada ya mwingine katika vumbi jekundu.

Porini ndovu wana adui wachache mno. Hata hivyo ndovu wa Tsavo kama tu wenzao kwingineko hawana mwendo wa kuwashinda wale wanyama katili — binadamu. Mwaka wa 2007, taifa lilipoteza tembo 47 pekee na kati ya mwaka wa 2008 hadi 2012, tembo 384 walichinjwa. Lakini hayo yote yamebadilika haraka sana — kuanzia Januari 2013 hadi sasa ndovu 221 wameuawa na wawindaji haramu.

Dkt. Patrick Omondi, Naibu Mkurugenzi anayesimamia uhifadhi wa wanyama pori katika Idara ya Wanyama (KWS) anajua vyema ukubwa wa hatari ya uwindaji haramu. Amechunguza idadi ya ndovu kwa miongo mingi. "Hesabu ya kwanza ya ndovu Kenya ilifanywa mwaka wa 1973 iligunduua kuwa tulikuwa na idadi nzuri ikiwa ndovu elfu 167 000. Miaka kumi na sita baadaye idadi hii ilikuwa imeteremka hadi 1600 ambayo ni hasara ya asilimia 80", alisema katika mahojiano na wanahabari.

Kifaru mweusi naye hajaendelea vyema. Kutoka idadi ya juu ya 20 000 mwaka wa 1973, wawindaji haramu wamewaangamiza hadi kufikia kiwango kidogo cha 300 mwaka wa 1989 ambayo ni kupungua kwa asilimia 90. Leo hii taifa lina idadi ya vifaru isiyozidi elfu moja katika maeneo yaliyolindwa ya mbuga ya Kitaifa ya Nairobi, Ziwa Nakuru na hifadhi za Lewa na Ol pejeta.

Matokeo haya ya kushangaza ya uwindaji haramu yalishtua serikali kuchukua hatua. Mwaka wa 1979, Shirika La Wanyama Pori (KWS) lilibuniwa kama chombo kamili kilicho na mamlaka ya kulinda kila kiumbe cha porini nchini.

Kikosi dhidi ya uwindaji haramu kilianzishwa pia kikiwa na magari na ndege. Visa vya uwindaji haramu vimepungua na wahalifu wakipigwa risasi papo hapo. Juhudi hizi zilizaa matunda na idadi ya ndovu ikapanda hadi idadi ya sasa 38 000.

Imetoholewa kutoka Ibrahim Mundi,"Siku za wawindaji haramu zimekwisha yasema KWS" *The Standard* (2013)



https://xtremepape.rs/